



Nini maana ya hali endelevu ya UVIKO?



World
PT Day
2021

Hali endelevu ya UVIKO awali inatafsiriwa kama uwepo wa viashiria na dalili zinazojitokeza mara baada ya kupata maambukizi ya virusi vya korona yanayoendelea kwa muda wa wiki 12 au zaidi.

Kwa kawaida, inajulikana kama hali ya awali ya UVIKO ndani ya wiki 4 na endelevu kuanzia wiki 4 hadi wiki 12.



Je hali endelevu ya UVIKO ipo?

Mgonjwa 1 kati ya 10 huonyesha uwepo wa dalili za UVIKO kwa kipindi cha zaidi ya wiki 12 au zaidi



Watu wengi waishio na ugonjwa wali-kuwa imara na wenye afya.



Watoto hupatwa na dalili endelevu za UVIKO sawa na watu wazima kwa kiwango kile kile.

Hali endelevu ya UVIKO huwaathiri watu waliolazwa kutokana na dalili za awali za UVIKO na wale waliopona wakiwa nyumbani. Watu walioapata maambukizi ya UVIKO kiasi au kwa kiwango kikubwa wanaweza kupata dalili endelevu za UVIKO.

Hali endelevu ya UVIKO ni ugonjwa ambao huathiri mifumo mbalimbali ya mwili; kuna dalili zaidi ya 200 zimeorodheshwa ambazo zinajitokeza kwa namna mbalimbali na hubadilika badilika kwa dalili zote zilizobashiriwa na zisizobashirika za kuibuka na kutulia.

Dalili za kawaida baada ya miezi 6 ni:



kuchoka kulikokithiri

dalili za uchovu mara baada ya kazi



kupoteza kumbukumbu na umakini

Dalili zinginezo ni:



kupumua kwa shida



maumivu ya kifua au kifua kubana



kushindwa kulala



mapigo ya moyo kuongezeka



kizunguzungu



maumivu ya misuli



maumivu kwenye viungo



msongo wa mawazo na wasiwasi



masikio kuuma



kuhisi kuumwa, kuharisha, tumbo kuuma, kukosa hamu ya kula



homa, kukohoa, kichwa kuuma, koo kuwasha, kutohisi halufu au radha ya chakula



vipele

Muafaka halijapatikana kimataifa juu ya maana halisi ya hali endelevu ya UVIKO. Japokuwa, kuna ongezeko la tafiti kuthibitisha ya kuwa hali hii ipo na inadhoofisha. Majaribio yamefanyika ili kuonyesha tabia za hali endelevu ya UVIKO ambayo inaathiri mifumo mbalimbali na kulemaza.



World
Physiotherapy

www.world.physio/wptday